# TUNGO REJESHI KATIKA KISWAHILI

R.D.K. Mekacha

Nia ya makala hii fupi ni kuibua mjadala miongoni mwa wanasarufi chipukizi wa Kiswahili, hususa walioko mashuleni na vyuoni, kuhusu sintaksia ya tungo rejeshi katika lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo tutajadili hatua za urejeshaji, namna tofauti ambazo urejeshaji hujidhihirisha katika Kiswahili, masharti na miiko inayoambatana na kila namna, na athari za urejeshaji katika mawasiliano kwa kutumia kiunzi cha Sarufi - Geuzi Żalishi(SGZ); kiunzi ambacho hakijatumika sana kuchanganulia sintaksia ya Kiswahili kwa Kiswahili. Tunatazamia kuwa baada ya kusoma makala hii wanasarufi chipukizi wanaweza pia kubaini utoshelevu na upungufu wa kiunzi hiki katika kuchanganua sintaksia ya tungo rejeshi za Kiswahili.

## I

Tungo rejeshi ni aina mojawapo ya tungo tegemezi (aina nyingine ikiwa tungo shamirishi)[1]. Tungo tegemezi ni sentensi iliyoshushwa hadhi na kutegemezwa katika sentensi nyingine. Hii ni kusema kuwa tungo tegemezi haitokei peke yake; bali hutokea kama sehemu ya sentensi, na kimuundo tungo tegemezi huwa kiambajengo ama cha sentensi kuu, au cha kiambajengo kingine cha sentensi hiyo.

Kwa mfano:

1. Mtoto ambaye alikuja jana ameondoka.

2. Mwalimu ameadhibu wanafunzi waliotoroka.

Katika sentensi 1 na 2 sehemu zilizopigiwa mstari ni tungo rejeshi.

Mojawapo ya sifa zinazotofautisha tungo rejeshi na tungo shamirishi ni kuwa siku zote tungo rejeshi hutegemezwa kunako kikundi nomino.[2] Hivyo kimuundo siku zote tungo rejeshi hutawaliwa na kifundo ambacho ni kikundi nomino. Ikiwa kikundi nomino(KN) ambacho kwacho tungo rejeshi imetegemezwa kinatawaliwa moja kwa moja na sentensi kuu, basi tungo rejeshi hiyo huwa sehemu ya sentensi inayofanya kazi kama kiima. Sentensi 1 ni mfano wa sentensi yenye tungo rejeshi ya aina hiyo. Lakini ikiwa

kikundi nomino ambacho kwacho tungo imetegemezwa kinatawaliwa na kikundi tenzi(KT) basi tungo rejeshi hiyo huwa sehemu ya sentensi inayofanya kazi kama shamirisho. Sentensi 2 ni mfano wa sentensi yenye tungo rejeshi ya aina hiyo.

Lakini kama tulivyoeleza awali tungo rejeshi ni sentensi iliyoshushwa hadhi na kutegemezwa katika sentensi nyingine. Hivyo, kimuundo, sentensi iliyotegemezwa sawa na sentensi nyingine, ina kikundi nomino na kikundi tenzi na hukiri kanuni ya msingi ya muundo wa sentensi(S) kuwa:

3. S -----> KN + KT[3]

Hii ni kusema kuwa katika kila moja ya sentensi 1 na 2 inazo walau sentensi mbili ndani yake kama inavyoonyeshwa hapo chini:

1 (a) Mtoto ameondoka (tungo kuu).
(b) Mtoto alikuja jana (tungo iliyorejeshwa).

2 (a) Mwalimu ameadhibu wanafunzi (tungo kuu).
(b) Wanafunzi walitoroka (tungo iliyorejeshwa).

Miongoni mwa sentensi hizo, sentensi 1(b) na 2(b) ndizo zilizoshushwa hadhi na 1(b) kutegemezwa katika 1(a) na 2(b) katika 2(a). Ikumbukwe, hata hivyo, kuwa sentensi 1(b) na 2(b) zimetegemezwa katika vikundi nomino vya sentensi 1(a) na 2(a) kwa mfuatano huo. Na kwamba sentensi 1(b) imetegemezwa kwenye kikundi nomino ambacho ni sehemu ya kiima ya sentensi 1(a) wakati sentensi 2(b) imetegemezwa kwenye kikundi nomino ambacho ni sehemu ya kikundi tenzi ya sentensi 2(a).

## II

Kwa kuwa sentensi 1(a) na 1(b) zinatokana na sentensi 1 ni dhahiri kuwa mtoto anayezungumziwa katika sentensi 1(a) ni yule yule anayezungumziwa katika sentensi 1(b). Vivyo hivyo wanafunzi wanaozungumziwa katika sentensi 2(a) ni wale wanaozungumziwa katika 2(b). Kwa maneno mengine kikundi nomino cha sentensi iliyotegemezwa ($KN_2$) hufanana na kikundi nomino ambacho kwacho sentensi hiyo imetegemezwa ($KN_1$):

4. $KN_2 = KN_1$

Ili kuondoa urudufishaji huo, hatua ya kwanza ya urejeshaji ni uwakilishi. Kikundi nomino cha sentensi iliyotegemezwa ($KN_2$) hubadilishwa: kibadala ambacho huchukua nafasi yake huitwa kiwakilishi. Viwakilishi ambavyo husimama badala ya kikundi nomino cha tungo rejeshi ($KN_2$) hurejea na kufanana na kikundi nomino kinachotawala kwa vile huakisi ngeli ya nomino ya kikundi nomino hicho. Jedwali ifuatayo inaonyesha viwakilishi hivyo mintarafu ya ngeli za nomino. Viwakilishi hivyo huitwa virejeshi (REJ).

| | Ngeli | Kirejeshi | Mfano |
|---|---|---|---|
| (i) | a | -ye- | Mtoto aliyetoroka ameadhibiwa. |
| (ii) | wa | -o- | Watoto waliotoroka wameadhibiwa. |
| (iii) | u | -o- | Mto uliofurika ni Mara |
| (iv) | i | -yo- | Miti iliyokatwa imekauka |
| (v) | li | -lo- | Jiwe lililotupwa limepotea |
| (vi) | ya | -yo- | Meno yaliyong'oka ni ya mbele |
| (vii) | ki | -cho- | kijiko kilichopotea ni cha mezani. |
| (viii) | vi | -vyo- | Viti vilivyoletwa havitoshi |
| (ix) | i | -yo- | Nguo iliyonunuliwa inambana |
| (x) | zi | -zo- | Nguo zilizochanika haziruhusiwi. |
| (xi) | u | -o- | Ubao ulionunuliwa unatosha |
| (xii) | zi | -zo- | Nyufa zilizozibwa zimetokea tena. |
| (xiii) | u | -o- | Ugonjwa ulioenea hautibiki |
| (xiv) | ya | -yo- | Magonjwa yanayoambukizwa huzuilika. |
| (xv) | ku | -ko- | Kuimba kulikofurahisha ni kwa Asha. |
| (xvi) | pa | -po- | Mahali palipofasifishwa hapatoshi. |
| (xvii) | mu | -mo- | Chumba mlimoingia nyoka kuna giza. |

Hatua ya pili ya urejeshaji ni uambishaji. Katika hatua hii kirejeshi huambishwa kwa namna tatu tofauti. Namna hizo za uambishaji wa kirejeshi ndizo msingi wa uainishaji wa miundo mbalimbali ya tungo rejeshi; nazo huitwa aina za urejeshaji.

Kwa aina zote tatu za urejeshaji, kama tulivyosema awali, lazima kiwakilishi kifanane na kurejea kikundi nomino kinachokitawala. Hii ni mojawapo ya sifa ambazo urejeshaji wa kila aina unazo. Sifa nyingine ni kuwa lazima kirejeshi kifuate mara tu baada ya kikundi nomino kilichorejewa. Ama kwa hakika, kama tutakavyoona hapa chini, ikitokea kirejeshi kuwa kimetengwa na kikundi nomino kinachorejewa, basi husogezwa(kwa kanuni geuzi)[4] ili kifuate mara tu baada ya kikundi nomino hicho. Hii ndiyo hatua ya tatu ya urejeshaji: hatua ambayo hutokea katika baadhi ya sentensi zenye tungo rejeshi.

Aina mojawapo ya urejeshaji huwa na umbo AMBA ambalo huambishwa kirejeshi mwishoni na kuwa na muundo:

5. AMBA + REJ[5]

Kwa mfano:-

6. Kitabu ambacho kilipotea kimeonekana.

7. Asha amepata adhabu ambayo haiwezi.

Aina nyingine ya urejeshaji huwa na kirejeshi ambacho huambishwa katikati ya viambishi awali kadha na mzizi wa kitenzi. Huwa na muundo:

8. + REJ +(ndani ya kifungutenzi.)

Kwa mfano:-

9. Mtoto aliyekuja jana ameondoka leo.

10. Mwalimu ameadhibu wanafunzi waliopiga kelele.

Aina nyingine ya urejeshaji huwa na kirejeshi ambacho huambishwa mwishoni mwa kitenzi, nacho huwa na muundo.

11. Kitenzi + REJ #

Kwa mfano:-

12. Wanafunzi wakosao huadhibiwa.

13. Vitabu tusomavyo ni vya kale.

IV

Kwa kuchunguza mifano iliyotolewa hapo juu, ni dhahiri kuwa muundo 11 una tofauti kubwa na miundo 5 na 8. Muundo 11 hutumika tu kwa hali ya mazoea. Kwa hiyo kitenzi ambacho kwacho kirejeshi kimeambishwa katu hakiambishwi mofimu ya wakati; au la sentensi inakua haikubaliki:

Kwa mfano:

12(a) *Wanafunzi wanakosao huadhibiwa.
13(a) *Vitabu tulisomavyo ni vya kale.

Aidha kitenzi cha hali ya mazoea hakitumiki pamoja na miundo 5 na 8 ya urejeshaji ambayo pia hubeba pia hubeba mofimu ya wakati; au la sentensi haikubaliki.

Kwa mfano:

12(b) *Wanafunzi ambao wakosao huadhibiwa.
13(b) *Vitabu tunavyosomavyo ni vya kale.

Miiko yote hiyo inayafinya sana matumizi ya muundo 11 wa rejeshaji, kiasi kwamba wako wanasarufi (kama Vitale 1981) wanaodai kuwa muundo huu ni wa nje na umetokana na muundo 5 ambao Vitale(1981) anadai ndiyo muundo wa ndani (wa msingi). Pia muundo huu unatofautiana sana na miundo mingine miwili. Miundo ya 5 na 8 inakaribiana kwa maana kuwa mtumiaji wa lugha huweza kutumia mmoja au mwingine baina ya miundo hiyo miwili kadri apendavyo kwani ni rahisi sentensi yenye muundo mmojawapo kubadilishwa na kuwa muundo mwingine.

Huu si ufujaji wa lugha, kwani tukichunguza kwa makini zaidi tutatambua kuwa siyo kila sentensi yenye urejeshi wa 5 (yaani urejeshi wa AMBA-) yaweza kuwa na urejeshi wa 8 (yaani urejeshi wenye kirejeshi kilichoambishwa kabla ya mzizi wa kitenzi).

Kwa mfano:-

14. Mwalimu aliyempiga mtoto ameadhibiwa.

Kwa kuwa nomino <u>mwalimu</u> na <u>mtoto</u> zote ziko katika ngeli moja, nazo huambatana na kirejeshi -ye-, basi katika muundo wa sentensi 14 kirejeshi -ye- chaweza kuhusishwa ama na <u>mwalimu</u>, au na <u>mtoto</u> na hivyo kuifanya sentensi

hiyo kuwa tata. Yaweza kumaanisha: ama mwalimu ndiye alimpiga mtoto, ama mtoto ndiye amempiga mwalimu. Ili kuondoa utata huo katika sentensi 14 lazima kutumia urejeshi wa 5 (wenye AMBA). Ukitumiwa tunapata sentensi:

14(a) Mwalimu ambaye amempiga mtoto ameadhibiwa.

Muundo wa urejeshaji wenye AMBA- hapa unafanya kazi mbili ili kuondoa utata. Kwanza unazisogeza zile nomino mbili zilizo katika ngeli moja mbalimbali na pia kirejeshi kinakuwa kimesogezwa katika nafasi ambayo kinahusishwa moja kwa moja na nomino inayorejewa. Muundo wa sentensi 14 ni ufuatao:

14(b) KN# REJ + KT# KN# KT

Lakini muundo wa sentensi 14(a) ni ufuatao:

14(c) KN# AMBA + REJ# KT# KN# KT

Kwa maelezo haya ni dhahiri kuwa muundo wa urejeshi wa 5 waweza kufanya kazi ambazo muundo wa 8 hauwezi. Yamkini ni kwa sababu hii ndiyo Vitale(1981) anadai kuwa huu ndiyo muundo wa msingi. Hoja hii yaweza kutupelekea kufikiri kuwa matumizi ya muundo huo (wa AMBA) hayana miiko. Lakini, kama tulivyoona awali, muundo huu hauwezi kutumika pamoja na hali ya mazoea. Aidha muundo huu hauwezi kutumika ikiwa mofimu ya wakati katika kirejeshi inafanana na ile ya tungo kuu. Kwa mfano tungo zifuatazo hazikubaliki:

15. *Mwalimu ambaye atampiga mtoto ataondoka.

16. *Mwalimu ambaye alimpiga mtoto aliondoka.

17. *Mwalimu ambaye anampiga mtoto anaondoka.

Matumizi ya muundo wa 8 wa urejeshi katika sentensi hizi yanazifanya zikubalike isipokuwa sentensi 17. Sentensi hiyo haitokubalika kwa sababu mtu mmoja hawezi kufanya matendo mawili kwa wakati uleule. Sentensi 15 itakubaliwa tu endapo itaongezewa mofimu ya hali ya matarajio.

Mabadiliko hayo yatatupa sentensi zifuatazo:-

15(a) Mwalimu atakayempiga mtoto ataondoka.
16(a) Mwalimu aliyempiga mtoto aliondoka.

Kwa kawaida miundo ya sentensi za Kiswahili kimsingi hukiri utaratibu wa kufuatana kwa kiima (K), Kitenzi (T), na Shamirisho (Sh). Tungo rejeshi pia hukiri utaratibu huu ikiwa kirejeshi ni sehemu ya kiima ama kiarifu. Lakini hutokea utaratibu huo kukiukwa na miundo ya tungo rejeshi.

Kwa mfano katika sentensi ifuatayo:-

18. Juma amekiona kitabu alichopoteza Ali.

Katika muundo wake wa ndani sentensi hiyo ina muundo ufuatao:-

18(a) *Juma ameona kitabu Ali alipoteza kitabu.
K T Y K T Y

Kirejeshi cha kitabu(ambacho ndiyo KN kinachojirudia) yaani -cho kikiambishwa katika kitenzi tunapata sentensi ifuatayo:-

18(b) *Juma ameona kitabu Ali alichopoteza.

Kirejeshi hicho kikiambishi kwenye umbo AMBA - Tunapata sentensi ifuatayo:-

18(c) *Juma ameona kitabu Ali alipoteza ambacho.

Sentensi 18(c) haikubaliki, na endapo sentensi 18(b) itakubalika basi ni tata, kwani haijulikani kiambishi ngeli -a- katika kitenzi poteza kinawakilisha nani kati ya Juma na Ali.

Kama tulivyosema awali budi kirejeshi hufuata mara tu baada ya kikundi nomino kinachorejewa kama inavyoonyeshwa hapa chini:

18(b) *Juma ameona kitabu alichopoteza Ali.
18(c) *Juma ameona kitabu ambacho Ali alipoteza

Matokeo ya usogezaji huo wa kirejeshi ni kutengua utaratibu wa mfuatano wa -KTY- katika tungo rejeshi. Mfuatano katika sentensi mpya unakua:

18. Juma ameona kitabu alichopoteza Ali
Y T K

18(d) Juma ameona kitabu ambacho Ali alipoteza
Y K T

Ukiukaji huu ukifanyika katika sentensi zenye urejeshaji wa kirejeshi ndani ya kifungutenzi na vikundi nomino vyote vitatu vikiwa na nomino za ngeli moja mawasiliano huathirika kwa maana kuwa kunazuka utata. Kwa mfano:-

19. Ali amemwoa msichana aliyemkataa Juma

Sentensi hii ina utata sawa na ule tuliouonyesha katika sentensi 14 hapo juu. Ili kuondoa utata huo wasemaji wa Kiswahili aghalabu hutumia kauli ya kutendewa katika kitenzi cha tungo rejeshi. Hivyo tunapata sentensi ifuatayo:

19(a) Ali amemwoa msichana ambaye amekataliwa na Juma.

VI

Katika makala hii fupi tumejadili hatua za urejeshaji, aina tatu za tungo rejeshi, masharti na miiko ya kila aina, athari za urejeshaji katika mawasiliano na kudokeza jinsi wasemaji wa lugha ya Kiswahili wanavyokabiliana na masharti, miiko na athari hizo. Kilichodhihirika wazi kutokana na uchanganuzi huu ni kuwa masharti na miiko ya miundo ya tungo haimfungi mtumiaji wa lugha: bali miundo hiyo hukunjwa, ikibidi, ili kukidhi haja ya mawasiliano. Matumaini yetu ni kuwa tumefanikiwa kuwachokoza wasomaji kuchanganua zaidi miundo ya Kiswahili na kupima utoshelevu wa kiunzi cha SGZ ambacho hata waasisi wake hivi sasa wanakitilia mashaka.

Maelezo

1. Rejea Wesana-Chomi(1973) na Vitale(1981)

2. Tofauti nyingine ni kuwa siku zote kifundo kinachotawala tungo tegemezi ni KN na kifundo kinachotawala tungo shamirishi ni KT. Pia katika ushamirishaji KT hicho lazima kiwe kile kinachofuatwa na KN.

3. Hii ni kanuni ya muundo wa vishazi(KMV) ambayo ndiyo msingi wa uchanganuzi wa miundo ya sentensi katika kiunzi cha SGZ

4. Kanuni geuzi(KG) hubainisha mabadiliko ya msingi ya miundo kama yalivyodhihirishwa na KMV.

5. Alama + inatumika kuonyesha mpaka wa mofimu, # mpaka wa neno, * sentensi isiyokubalika, au ambayo bado haijakamilika.

MAREJEO:


Culicover P.W. (1976) Syntax, Academic Press Inc; New York.

Jacobsen B.; (1977) Transformational Generative Grammar, North-Holland Publishing Company, Amsterdam.

Kayuza J.C. (1977) "Miundo ya Sentensi za Kiswahili" makala, haijachapishwa, Chuo cha Ualimu, Dar es Salaam.

Mkude D.J. (1983) "Uchambuzi wa Sentensi za Kiswahili" Lugha ya Kiswahili, TUKI, Dar es Salaam

Soames S. na Perlmutter D.(1979) Syntactic Argumentation and the Structure of English, University of Carlifornia Press, Cerkeley.

Vitale A.J. (1981), Swahili Syntax, Foris Publications, Cinnaminson, U.S.A.

Wesona-Chomi E.; (1973) "Towards The Syntax of Complex Sentences in Swahili" katika Kiswahili Tol. 43/2, Dar es Salaam.

Wesana-Chomi E; (1983) "Preliminaries to Adverbial Complementation in Swahili", Makala haija-chapishwa, Dar es Salaam.